**JINA……………………………..……………….NAMBA YA MTAHINIWA………...…**

**SAHIHI YA MTAHINIWA……………………….. TAREHE………………………………..**

**KIDATO ………………………………………………………………………………………..**

**MTIHANI WA PAMOJA WA SUKELLEMO 2022**

**102/3 KISWAHILI Karatasi ya 3**

**FASIHI**

**Muda: Saa 2 ½**

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

**MAAGIZO**

1. *Jibu maswali manne* ***pekee****.*
2. *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima***
3. *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya Hadithi fupi,Tamthilia na Ushairi.*
4. *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*
5. *Kila swali lina alama 20*
6. *Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1.** LAZIMA

**a. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Mabibi na mabwana, ndugu na marafiki hamjambo! Nimefika hapa leo kushuhudia sherehe za vijana hao wanaofuzu kuingia utu uzimani. Tangu jadi mababu zetu waliandaa sherehe kama hizi ili kuwaandaa vijana wao kukabiliana na maisha ya usoni. Wanangu, utu uzima hautokani tu na viviga au kisu cha ngariba. Ni matendo na tabia. Naam, ni matendo na tabia. Katika jamii ya sasa watu humpima mtu kutokana na ufanifu wake kiuchumi, kielimu na kijamii. Mtu asiye na mali yake hubezwa kwa kutofanya bidii inavyostahili. Hivyo basi, nawashauri vijana wanaofuzu leo kuwa, mnafaa kutia bidii masomoni ili mustakabali wenu uwe mzuri. Katika nyakati zetu, ubingwa wetu ulipimwa katika fani ya vita na ngoma. Ungewasikia wanaume wakijisifu kwa wimbo wakisema:

Ooh ooh ooh!

Mimi ni chuma inayoishi

Ningiapo vitani, macho yangu tu huwafisha wengi.

Viganja vyangu vimeiletea jamii yetu fahari

Wananiita Ngao.

Juzi ngomani niliwapiku wote

Wanawali waliniangukia kwa kutaka uchumba

Nani mwingine kama Ngao?

Hata hivyo, hali katika jamii ya sasa ni tofauti. Ngoma imekuwa nyenzo ya burudani tu. Navyo vita vya kikabila vimepitwa na wakati. Wanaopigana aghalabu huchukiliwa hatua kali za kisheria. Elimu ni silaha ya pekee. Elimu itawafungulia milango ya heri. Ndugu na marafiki, nawaomba nyote muwasisitizie vijana hao umuhimu wa kuwatii walimu wao na kutia bidii masomoni watakaporudi shuleni. Msisite kuwaadhibu wanapokosea. Ni muhimu kukumbuka kuwa, mchelea mwana kulia hulia mwenyewe. Tulisimuliwa na bibi kuwa, hapo zamani Za kale mwanamke fulani alificha mnyama hatari aliyekuwa akifukuzwa na mashujaa wa jamii. Baada ya mashujaa hao kuondoka, mnyama huyo alimla mwanamke huyo. Ingawa ni hadithi, kisa hicho kinatufunzwa kuwa, hatufai kuficha matendo mabaya ya wanetu. Tuwarekebishe mapema. Nikimaliza naomba kuwajuza vijana hawa kuwa, tohara siyo ufunguo wa ulevi. Inahuzunisha kuwakuta vijana wadogo wamelala matopeni kwa kushindwa kutembea kutokana na ulevi. Wengine hubaki pale hadi asubuhi wakitumbuizwa na milio ya vyura. Nina matumaini kuwa, kundi hili litakuwa tofauti. Asanteni kwa kunisikiliza.

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

**Maswali**

i. Tambua kipera cha utungo huu. (alama 1)

ii. Eleza sifa za kipera ulichotaja katika (i) (alama 4)
iii. Eleza toni inayojitokeza katika kifungu hiki. (alama 2)
iv. Fafanua mbinu za kimtindo zinazodhihirika katika kifungu hiki. (alama 3)

b. Nyumbani mwetu mna papai lilioiva lakini siwezi kulichuma – ndugu wa kiume asimuoe nduguye wa kike.

i. Bainisha kipera kinachorejelewa. (alama 1).

ii. Andika shughuli moja ya Kijamii na moja ya Kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. (alama 2)

iii. Unakusudia kukusanya data kuhusu kipera hiki. Eleza manufaa ya kutumia hojaji. (alama 4)

iv. Kipera hiki kinazidi kufifia katika jamii yako. Pendekeza mbuinu zozote tatu ambazo jamii hiyo inaweza kutumia kuzuia hali hii. (alama 3)

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

**<u>SEHEMU B: RIWAYA YA CHOZI LA HERI ; Assumpta Matei</u>**

***Jibu swali la 2 au 3***

2.

a. "Inasikitisha kwamba badala ya kuliongoa jahazi letu wameligongesha mwamba bila kujua."

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii. Taja mbinu zozote **mbili** zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

iii. Eleza sifa zozote **nne** za msemaji. (alama 4)

b. Tathmini umuhimu wa dayolojia kati ya Ridhaa na Tila katika kuvikuza vipengele vifuatavyo :

i. Maudhui (alama 5)

ii. Wahusika (alama 5)

3.

a. Jadili mtindo kwenye dondoo lifuatalo : (alama 8)

Jua linalochomoza halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua.

Tukio hili linafuatwa na umeme, kisha mtutumo wa radi. Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; matone yanayoanguka kwenye ngozi laini za wanangu wakembe, Lime na Mwanaheri. Nawatazama kwa imani lakini siwezi kuwasaidia. Sina hata tambara duni la kuwafunikia. Linalobaki ni kumshuru Mungu kuwa tungali hai. Ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu,Subira. Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu kwani huyu siye Subira wangu wa zamani. Siye, siye, siye-e-e-e. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha, kikwi. Tazama tambo lake lililoumbuka. Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira! Haya ni matokeo ya ubahaimu wa binadamu. Kwa mbali namwona Ridhaa – mwamu hasa – akitafuna kitu fulani, nadhani ni mzizimwitu. Ridhaa, kweli Ridhaa kula mzizi! Daktari mzima! Mkurugenzi mzima wa Wakfu wa Matibabu nchini! Wanasema wajuao kuwa simba akikosa nyama hula nyasi. Msafiri kafiri ati! Amekosa la maama, hili la mbwa ataliamwa!

b. Onyesha vile utu wa mtu ulivyopujuliwa kwa kurejelea Riwaya ya *Chozi la Heri*. (alama 12)

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

**SEHEMU C: TAMTHILIA; KIGOGO – Pauline Kea**

***Jibu swali 4 au 5***

4. "Mimi ni mtu wa vitendo si wa vishindo"

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama4)

b. Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza maudhui. (alama 4)

c. Eleza namna Pauline Kea alivyofaulu kutumia mbinu ya ***ishara*** katika kufanikisha maudhui. (alama 12)

5. Tamthlia ya *Kigogo* inamulika hali halisi katika mataifa mengi ya Afrika. Jadili. (alama 20)

**SEHEMU D: USHAIRI**

*Jibu swali 6 au 7*

6. SIPENDI KUCHEKA

Pana jambo linatukiya, kwangu hilo ni muhali
Kitenda naona haya, kujishusha yangu hali
Sipendi unipe hidaya, sipendi kutenda hili
Sipendi mimi kucheka

Sipendi mimi kucheka, kuchekea mawa
Sipendi ya dhihaka, kwangu nyemi hiwi
Sipendi kwa hakika, mwovu kistawika

Halafuye nikacheka!
Maskini akiteswa
Yatima akinyanyaswa
Mnyonge naye akinyonywa
Sipendi hata ikiwa
Unazo nguvu najuwa
Ni hili sitatekezwa

Mbona lakini nicheke, kwayo furaha?
Na wewe ukajiweke, uli na siha
Na yatima pweke, wa anahaha?
Amenyimwa haki yake, hanayo raha!
Na moyo wangu ucheke, kwa ha! ha! ha!
Kucheka kwa kuchewa mimi katu sitacheka.

**MASWALI**

a) i. Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)

ii. Thibitisha jibu lako la (a i ) hapo juu kwa kutaja mifano mitatu. (alama 3)

b) Kwa nini mshairi wa shairi hili hataki kucheka. (alama2)

.

c) Eleza umbo la ubeti wa tatu wa shairi hili. (alama3)

d) Tambua nafsineni na nafsinenenwa katika shairi hili. (alama 2)

e) Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)

f) Dhihirisha umuhimu wa uhuru ufuatao katika shairi hili. (alama 2)

i. Tabdila

ii. Kuboronga sarufi.

g) Jadili jinsi mwandishi wa shairi hili ametumia istilahi za lugha. (alama 2)

h) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari/tutumbi. (alama 3)

7. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Watalamu muwe macho, uani moto muenge,
Muenge hicho ambacho, cha watu wenye mawenge,

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

Mawenge yenye kijicho, Kiswahili wakivunge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Sichafue Kiswahili, barakala tuwapinge,
Tuwapinge kila hali, wasiguse tuwainge,
Tuwainge wende mbali, Kiswahili tujijenge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Sichafue yetu lugha,waharibu wabanange,
Wabanange iwe nyagha, waiweke tengetenge,
Lugha kuitwa ulugha, lafudhi watia denge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Tuichangie heshima, na ulugha tuupinge,
Tuhifadhi kwa salama, na kisingio unyonge,
Kelele za maamuma, sio watu ni visinge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Kasema Sheikh Amri, Kiswahili tukisenge,
Kisitawi kinawiri, kitumike kwenye bunge,
Hii ni yetu fahari, lugha yetu tuichunge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Kikipatwa na maradhi, kwa sindano tukidunge,
Kila jama kukitidhi, kipatwe hapo tupunge,
Tukitia mfawadhi, kama kunde na kihenge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

**Maswali**

a) Bainisha mapendekezo manne yanayodokezwa na mshairi kuhusu kuhifadhi na kuimarishalughɛ ya Kiswahili. (alama 4)

b) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)

c) Bainisha nafsi nenewa na nenwa katika shairi hili. (alama 2)

d) Eleza mbinu mbili ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)

e) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 2)

f) Bainisha bahari mbili za ushairi zinazojitokeza katika ubeti wa kwanza na wa pili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama 4)

   i. Vipande katika mishororo

   ii. Mpangilio wa maneno.

g) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika ushairi: (alama 2)

i. Mfawadhi
ii. Barakala
iii. Maamuma
iv. Muenge

**<u>SEHEMU E: HADITHI FUPI; TUMBO LISILOSHIBA NAHADITHI NYINGINE – Alifa Chokocho na Dumu Kayanda (Wh)</u>**

8.

*a. Mtihani wa Maisha*

… walitoka ndani ya ofisi ya mwalimu mkuu wakitabasamu huku machozi yanawatoka. Mtu angesemaje ati? Wanafurahi na wakati huo huo wanasononeka? Wamefaulu mtihani au wamefeli? Wanachanganya watu au wamechanganyikiwa? Haidhuru, Samueli alijisemea kimoyomoyo kwamba yeye atakuwa na moyo zamu yake itakapofika. Atapokea ya kupokea liwe liwalo kwani yeye ni mwanamume. Akitoka ndani atakuwa akitembea kama fahali.

i. Tathmini mitindo iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 5)

ii. Eleza umuhimu wa Samueli katika kuendeleza ploti ya Hadith husika. (alama 5)

*b. Shibe Inatumaliza*

"wanafanya kazi ya ukwe tu. <u>Hawana wasichofaya lakini hawana wafanyacho."</u>

Kwa hoja sita, thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari huku ukirejelea hadithi *Shibe Inatumaliza.* (alama 6)

*c. Tulipokutana Tena*

"Hivi ndivyo maisha yapasavyo kuwa- huru kabisa."

Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

*MWISHO*

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com